Ecolebooks.com

MUHULA WA PILI
KINDATO CHA KWANZA

MARKING SCHEME

UFAHAMU (ALAMA 15)
MADHARA YA SIGARA.

(a) Mwaka wa 1598 A.D. (ala 1)

(b) Denmark, Uholanzi na Sweden (ala 1)

(c) (i) Kila sekunda ipitayo mtu mmoja anafariki kutokana na madhara ya tumbaku.

(ii) Uvutaji wa sigara unasababisha magonjwa mengi kama vile saratani ya mapafu, wendawazimu, kupooza, matatizo ya mfumo wa hewa, kunyonyoka nywele, kupungua kwa nguvu za kiume, maradhi ya ngozi na mengineyo.

(iii) Mvutaji sigara hutoa harufu mbaya mdomoni.

(iv) Akili za mvutaji sigara huathirika kutokana na chembechembe za ulevi zilizomo kwenye sigara.

(v) Unaathiri ukuaji wa mimba kwa mama mjamzito. (ala 5)

(d) (i) Mishipa inayosafirisha damu katika moyo huathirika.
(ii) Watoto hao huishia kuvuta sigara.
(iii) Wanakosa maadili.
(iv) Watoto wa mvutaji sigara huzaliwa wakiwa na uzito pungufu. (ala 4)

(e) (i) Kila mwaka Shirika la afya Ulimwenguni hutenga siku maalumu ya kuelimisha jamii kuhusu athari za kiafya na madhara yatokanayo na matumizi ya tumbaku. Pesa hutumika katika maadhimisho haya.

(ii) Pesa nyingi zinatumika kutibu magonjwa yanayotokana na athari za uvutaji sigara.

(iii) Uvutaji sigara husababisha vifo vingi vya watu wanaotegemewa katika jamii. (ala 2)

(f) (i) Kupooza – Kukosa hisia katika sehemu ya mwili kama vile mguu au mkono.

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

(ii) Maadhimisho – Sherehe ya kukumbuka tukio Fulani. (ala 2)

LUGHA

(a) (i) Irabu ni sauti ambazo hutamkwa bila hewa kuzuiliwa.

(ii) Konsonanti ni sauti ambazo zinapotamkwa hewa huzuiliwa.

(b) (i) Kiimbo ni kupanda na kushuka kwa mawimbi ya sauti mtu anapozungumza.
(ii) Shadda ni mkazo unaowekwa kwenye silabi fulani ya neno ili neno hilo liweze kutokeza maana yake halisi.

(c) (i) Sentensi
(ii) Neno
(iii) Silabi
(iv) Sauti

(d) (i) Mabati yamenunuliwa
(ii) Baba amekwenda dukani

(e) (i) Nchi za Afrika mashariki hazilemewi na madeni
(ii) Mbu hajamuuma mtoto
(iii) Baba hajaandika barua ndefu

(f) (i) Ulipendelea kula nyama siku hizo
(ii) Opiyo alipenda kujiingiza katikati kama mchuzi wa ugali

(g) (i) Maziwa ya watoto yalimwagwa na paka wale
(ii) Uvivu wa kina Juma unakera

(h) (i) Nenda sokoni ukaninunulie sukari, maziwa na mkate.
(ii) Maadam umeshafika tuanze mkutano ?

(i)

NAFSI	WAKATI	KIREJESHI	KITENDWA	MZIZI	KIISHIO
A	li	ye		lim	a
A	li	ye	m	pig	a
A	na	o	u	pand	a
A	li			pik	a

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

ni	ta	vi		let	a

(j) (i) Hadithi
(ii) Maigizo
(iii) Ushairi
(iv) Semi

(k) (i) sana
(ii) Kesho jioni

(l) (i) Pigiwa
(ii) Jengewa
(iii) Fagiliwa
(iv) Chorewa

(m) (i) Humsaidia binadamu kuyaelewa mazingira yake. Tunahitaji lugha ili kuvipa majina vitu vinavyopatikana katika mazingira yetu kwa mfano: Miti, viroboto, ng'ombe

(ii) Kupitia kwa lugha binadamu wanaweza kushirikiana na kuwasiliana kwa mema au mabaya basi kusaidia katika utatuzi wa migogoro.

(iii) Huwezesha ushirikiano baina ya watu binafsi au hata kati ya nchi na nyingine kwani unategemea mawasiliano ya kimazungumzo ya moja kwa moja au kwa maandishi.

(n) (i) Mchoraji yule huchora picha nzuri.
(ii) Mpishi hupika chakula kitamu.

(o) Salaala ! Majangili wamewaua ndovu kumi leo asubuhi
I N T N V E E

Wale watafungwa
W T

FASIHI

1. Kuelimisha – Fasihi huwa na mafunzo mengi / maadili ya tabia nzuri.
2. Kuburudisha
3. Kuelekeza
4. Kuonya na kushauri

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

5. Kukuza uwezo wa kufikiri
6. Kuendeleza utamaduni

FASIHI SIMULIZI	FASIHI ANDISHI
(i)Huwasilishwa kwa njia ya mdomo (ii)Huhifadhiwa akilini (iii)Huweza kubadilishwa msimulizi anapowasilisha jukwaani. (iv)Ni mali ya jamii. (v)Hadhira yake n hai	(i)Huwasilishwa katika maandishi (ii)Njia ya kuhifadhi ni kwa maandishi (iii)Maandishi yaliyoandikwa hayabadiliki. (iv)Ni mali ya mtu binafsi (v)Hadhira haina mchango wa moja kwa moja.

ISIMU JAMII

(a) Ni lugha ya matangazo ya biashara (alama 2)

(b) (i) Inatoa habari maalum kwa mfano, kuwa sabuni ya Gresha ni mpya, ina harufu nzuri, inang'arisha na bei yake ni nafuu.

(ii) Inachanganya msimbo – Kiingereza na Kiswahili kwa mfano 'It is new!'

(iii) Lugha si sanifu, kwa mfano, *harufu poa.*

(iv) Ina kukariri kwingi ili kusisitiza ujumbe, kwa mfano maneno sabuni *ya* 'GRESHA' na '*nunua*' yamekaririwa.

(v) Lugha yake ni nyepesi na inaeleweka kwa urahisi.

(v) Huwa na porojo na kelele nyingi ili kuwavutia wateja.

(vi) Matangazo yanaweza kuandamana na picha na muziki ili kufanya yapendeze na kuvutia zaidi hivyo kila mtu kuvutiwa kununua bidhaa hiyo.

(vii) Inaweza kuwa na kuhamisha ndimi.

(viii) Lugha hii hutaja bei ya kile kinachotangazwa. Kwa mfano, *'Bei yake ni shilingi 20/= tu.'*

(ix) Ina ushawishi mwingi, kwa mfano, *'Bei yake ni nafuu', Kila mtu ainunua'.*

(x) Ina chuku sana ili kumvutia mteja. Kwa mfano, *'inadumu siku yote, inalainisha ngozi.'*

*(*alama 8)

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

INSHA

Mtahiniwa azungumzie maisha yake. Safari ya maisha

(i) Awe na shida katika maisha hayo.
(ii) Afanye juhudi ili kujitoa katika shida hizo.
(iii) Aweze kupata mafanikio hatimaye.

Atakayeongeza maneno katika kimalizio aondolewa maki 2.

Atakayekosa kutumia maneno yote katika kimalizio aondolewe maki 2.

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM